


WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI



SEKTA YA UVUVI

**ATHARI ZA UVUVI HARAMU
WA KUTUMIA MABOMU**



UVUVI HARAMU

Kuna aina nyingi za uvuvi haramu:

- (i) Matumizi ya nyavu zenyenye macho madogo
- (ii) Kupiga katuli
- (iii) Matumizi ya Sumu
- (iv) Matumizi ya vilipuzi ikwemo mabomu yaliyotengenezwa kwa baruti

(i) Matumizi ya nyavu zenyenye macho madogo:

Ni matumizi ya nyavu zenyenye macho madogo chini ya Inchi 3 katika ukanda wa wa Pwani na maziwa mengine na chini ya nchi 6 katika Ziwa Victoria. Vilevile matumizi ya nyavu zenyenye macho madogo chini ya Milimita 10 katika uvuvi wa dagaa katika ukanda wa pwani na baadhi ya maziwa na matumizi ya nyavu chini ya Milimita 8 katika ziwa Victoria. Aidha katika Uvuvi wa Kambamiti ni matumizi ya nyavu zilizo chini ya Milimita 1.5.

(ii) Kupiga Katuli

Ni kitendo cha kuwalazimisha samaki kuingia katika mtego kutoka katika mazingira yake ya asili.

(iii) Matumizi ya Sumu

Ni matumizi ya sumu ya viwandani au mimea (Utupa) katika uvuvi wa Samaki.

(iv) Matumizi ya Mabomu

Ni matumizi ya vilipuzi ikiwemo mabomu yanayotengenezwa kwa baruti. Uvuvi huu wa kutumia mabomu huathiri matumbawe.

UVUVI HARAMU WA KUTUMIA MABOMU HUATHIRI MATUMBWE.

Umuhimu wa matumbawe

Matumbawe ni moja ya viumbe waishio kwenye maji katika bahari. Matumbawe haya ni muhimu kwa ajili ya mazalia na makulio ya samaki. Vilevile matumbawe ni maeneo ambayo muhimu kwa ajili ya utalii ikolojia.



(A) Matumbawe ambayo hayajaharibiwa



(B) Matumbawe ambayo Hayajaharibiwa

UHARIBIFU WA MATUMBWE HUTOKANA NA UVUVI HARAMU WA KUTUMIA MABOMU

Uvuvi wa kutumia mabomu ni uvuvi haramu uliokatazwa kisheria. Wavuvi wenye ulafi wa kupata samaki kwa wingi na mara moja hutumia mabomu na kuyalipua kwenye maeneo ya matumbawe ambapo ni mazalia na makazi ya samaki aina mbalimbali.

Bomu linapolipuliwa kwenye maeneo ya matumbawe huathiri matumbawe, samaki na viumbe wengine wa baharini pamoja na eneo lilolipuliwa.



Mlipuko Wa Bomu na Matokeo Yake

Uoto wa matumbawe Katika maeneo yaliyolipuliwa huharibika na mara nyingi hauoti tena na hivyo kuondoa mazalia na makulio ya samaki husika.



Matumbawe Yaliyoharibiwa na Bomu Yakionesha pia Kutokuwa na Samaki

Athari nyingine zinazotokana na uvuvi haramu wa kutumia mabomu ni pamoja na mtumiaji wa mabomu hayo kupoteza baadhi ya viungo vya mwili wake au hata kupoteza uhai wake kabisa



Mvuvi Aliyekatika Mikono Kutokana na Uvuvi Haramu wa Kutumia Mabomu

IMEANDALIWA NA:

Wizara ya Mifugo na Uvuvu;
Sekta ya Uvuvu
S. L. P. 2847
40487 DODOMA
Simu Na: 255 026 2322 613
Nukushi: 255 026 2322 611
Barua pepe:ps@mifugouvuv.go.tz